# Maelezo Mafupi Ya Mafundisho Ya Mungu.

**Yatakayoongelewa:**
**Upendo wa Mungu.**
**Uhalisi Wa Mungu**
**Thamani ya Kuwepo kwa Mungu.**

Mungu muumbaji na mwenyeenzi ametuletea manenoya uvuvio (1Tim.3:15 -17) ambayo haitakiwi kutafsili kwa kadiri mtuapendavyo (2 Petro 1:20) neno ambalo laweza kumkamilisha mtu (Yoh. 17:17) iwapo mtu atasikia na kutii (Yoh. 12:48) sauti ya muumba, kwa kupitia neno hilo,tunaye Mungu sio kujaribu kuthibitsha kuwa Mungu yupo ila anajidhihilisha,uwepo wake,basili yake na uhusika wake ili tuweze kutamani kuwa watakatifu (1 Pet. 1:16).

Imeelezwa kwamba mtu anaona uhitaji wa kuabudu na kuheshimu kitu ambacho ni kikubwa kuliko yeye, kupitia hatua zote za maendeleo na jamii zote toka mwanzo kila kundi linawajibu kuelewa, kufuata, kuabudu, kusihi na kuiga ili kwamba imani yao iwe kwa kitu kikubwa, Imani zote hizo japo ni tofauti bado ni moja kati ya asil na agano lake laweza kufahamika kwa kumwaga damu hapo mambo yataendelea vizuri uwiano huu unaweza kutudhihilishia kwamba binadamu anachokiungo cha imani moja .

Mtu anapotambua udhaifu wake na kufikili kuwa kwa kumwaga damu kwaweza kusawazisha mambo Je, mtu huyo aliwezaje kutambua udhaifu huo na akifikili kuwa haya ni sawa? .Kwa sababu binadamu alipoasi, aliweza kutambua kuwa roho yake imepanuka kwa uwezo mkubwa na akaona utupu wake (Mwa. 3:8) . Uwezo utokao juu ulipotokea na akaongea na huyo binadamu na kumlaumu kwa dhambi yake kasha Mungu alimpa huyo binadamu kanuni ya kumwaga damu ya mnyama kama sadaka ya kuteketezwa ili kuziondoa dhambi zake (Ebr. 9:12-13; Mwa. 4:3-4; 8:20-22)

Tunapochunguza mfano wa imani tunaweza kuona kuwa kila jamii inapata msingi wa imani kutoka kwa mababu ambapo ufuata kupitia kwa kufundishwa na watu kama Abraham, Ayubu, Isaka na wengine waliotumwa na Mungu (Ebr. 1:1). Kama vile Mungu alivyokamilisha utashi wake katika Mwa. 3:15, alianza kubaliki mbegu ya kabila dhidi ya mataifa mengine. Kwa kufanya hivyo sio kwamba Mungu alikuwa anawachukia mataifa mengine ya dunia hii isipokuwa Mungu alichoona ili alete kwake mwana. Hivyo ungekuwa mwanga wa kungaza kwa watu wote ili watu wote waweze kuja kwake (Eze. 5:5-6). Kwa kuwa Israeli waliochaguliwa na Mungu walishindwa kumfuata na Mataifa mengine nayo pia wakaendelea kupotea toka kwenye utaratibu wa Imani ya mababu zao. Hata hiyo msingi wa imani uliendelea kulindwa wakati wote.

Kwa mfano karibu kila kabila walikuwa na mji mtakatikfu, mtu mtakatifu ambaye angeendelea kutoa sadaka ama tambiko kwa wale ambao wanataka kusamehewa ama kupata baraka, Misingi. Hiyo haikubadilika, japo kuna mawazo ya baadhi ya wamishonari wa kwanza ailiyekuwa akitafuta umaarufu na hazina kufikili kuwa baadhi ya makabila hawana Mungu wala hawana kanuni za dini. Lakini baadae wapelelezi na wamisionari waliokaa muda mrefu na makabila wanadhibithisha kuwa makabila yote yana dini au miungu na mafundisho yao na maangano yao japokuwa ni tofauti na neno la Mungu.

Inaoneka kuwa misingi hii kwa mafundisho yao na maagano vinatokana na umoja huo wa zamani wa mababu uliotolewa na mwenye enzi binadamu alijifunza udhaifu wake na kujaribu kufanya mambo vyema, hiyo imefanyika kwa kuwa mwenyeuwezo mkuu amemwonyesha mwanadamu dhambi yake (Mwa. 3:9-12)

Kwa kuwa watu wanayo aina ya imani kwa Mungu (Rum. 1:8-17) inaonekana kitabu cha Mungu yaani Biblia kimetolewa ili kutuongoza kumrudia Mungu ambaye hapo kale mababu zetu walimjua kisha wakaanguka kwa kufuata tamaa zao wenyewe. Tunaweza kumwu liza Mungu jina lake kama vile Musa alivyofanya ili tuone sura yake, tuna alama na maajabu ilitukadhibitishe uwepo wake hata hivyo amedhibitisha uwepo wake kupitia Biblia na uumbaji uwepo wake umedhibitika kupitia katika historia ya mwanadamu na utafiti. Uwepo wake umedhibitshwa na uwepo wa vilima, mabonde, mito, upepo,

mawimbi, mbingu na sayari  mawazo yetu na roho zetu zinatusuku ma kuwa yupo Mungu (Mwa. 1:1). Bila shaka mtu yeyote akiangalia ushuhuda wake na historia yetu na bado akasema kuwa hakuna Mungu mtu huyo lazima  awe mpumbavu. (Zab. 14:1)

**Asili ya Mungu.**

Japo Mungu hajajiweka yeye kuweza kudhibitisha uwepo wake. Laki ni ametuonyesha asili yake kwa uvuvio wa neno lake. Tunajifunza kutoka kwenye maneno yake kuwa Yeye ni Roho (Yoh. 4:24) na ni mwanga (1 Yoh. 1:5). Hana umbola kimwili ila aweza kuvaa umbo lolote kama apendavyo (Waf. 2:7) na bado akawa mzima kama sisi tulivyo  leo. Lakini zaidi yetu yeye ni wa milele ni mwuumba wa mbingu na nchi.

Kwa kuona kuwa Mungu ni roho na kuwa tumeumbwa kwa mfano wake, tumeumbwa na umbo lenye mwili na damu. Vilele tuna Roho ambayo itaishi milele. Hilo lina tuthibitishia tuelewe kuwa na jinsi gani tulivyoumbwa katika mfano wake Mwa. 1:27; 5:1. Ndio kusema roho zetu zipo kama yeye undani na uweza wa Mungu upo, ni safi, Unaongea, Unatubu, Unaonya, Unapenda, Unachukia, maneno yake yanathibitisha yote hayo (1Thes. 5:21).

Uhalisi wa Mungu upo katika hali tatu tafauti lakini katika utambulisho mmoja tunaye Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu vyote vina kazi tofauti lakina lengo moja (1 Yoh. 5:6-8) kufanya kazi kwa matumaini ya kurudisha binadamu kwa Mungu.

**Thamani Ya Kuwepo Kwa Mungu.**

Katika kitabu chake tunajua kuwa Mungu hajaweka ili kuthibitisha kuwepo kwake, hata hivyo anatuonyesha thamani  ya kuwepo kwake ambayo ni Kiroho. Inatuonyesha  kuwa anayo mamlaka yote( Ufu. 19:6) mbinguni na duniani (Mat. 28:18) anatuonyesha kuwa anajua yote (Isa. 40:28) hanitaji mtu kumwambia kuhusu mtu mwingine (Yoh. 1:5) kupita haki yake ana upendo anafanya kazi kwa kila mtu (Ufu. 16:7) Mungu ni pendo (Yoh. 3:16) na Mungu wa amani (Rum. 1:7) anao uwezo kiasi kwamba hawezi kudanganywa (Tit.1:2) wala hawezi kujaribiwa (Yak.1:130) Yeye ni mkamilifu katika njia zote (Zab. 99:9) Thamani hiyo na zaidi ni kubwa kuliko Mungu mwingine yeyote ambaye binadamu amewahi kufanya kama Daudi alivyowaambia Israel, Mungu Bwana wetu ni Bwana mmoja,  Tuishi kujifunza yaleyale hata leo.